



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS, UTUMISHI NA UTAWALA BORA
WAKALA YA SERIKALI MTANDAO

Samora, Avenue, ExTelecoms House, 2nd Floor, P.O Box 4273, Dar es Salaam, Tel: +255222129868/7
Fax: +255222129878, General eMail: info@ega.go.tz, CEO eMail: ceo@ega.go.tz, Website: www.ega.go.tz



TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

Taasisi za umma zinashauriwa kushirikiana na Wakala ya Serikali Mtandao katika kupanga na kutekeleza Miradi ya TEHAMA Serikalini ili kurahisisha mpango wa kubaini na kuondoa urudufu na kuipunguzia Serikali gharama za usimikaji na uendeshaji mifumo inayofanana ndani ya Serikali.

Kutokana na utaratibu huo, taasisi yoyote ya umma inayotaka kuanzisha mradi wa TEHAMA inatakiwa kuwasilisha mradi huo ukiwa unaendana na vigezo vilivyowekwa katika orodha hakiki ya miradi ya TEHAMA Serikalini, inayopatikana katika tovuti ya Wakala www.ega.go.tz, kwa Wakala ili uweze kuhakikiwa na kuthibitiswa.

Aidha, mradi huo unatakiwa kuonyesha jinsi gani utaboresha utendaji kazi wa taasisi husika, utoaji wa huduma kwa umma ikilinganishwa na utaratibu wa zamani na iwapo unatimiza malengo ya Dira ya Taifa ya Mandeleo 2025 na unazingatia Sera, Viwango, Miongozo na Taratibu za Serikali.

Pia, Mradi huo unatakiwa kuonyesha mpango wa uanzishaji kwa kuainisha ufadhili, umiliki, majukumu, kazi zitakazofanyika, muda utakaotumika katika utekelezaji, vyanzo vya gharama za uendeshaji mradi huo na ushirikishwaji wa wadau pamoja na watekelezeji wa ndani ya taasisi hiyo.

Ili kupunguza urudufu na gharama za uendeshaji wa miradi ya TEHAMA, mradi huo unatakiwa kuonesha uhusiano uliopo kati ya jitihada hiyo na nyingine za aina hiyo zinazotekelezwa katika taasisi za umma. Pia mradi huo unatakiwa kuonyesha aina na mtindo wa teknolojia inayotumika, kama ni rafiki kwa watumiaji na ni endelevu kwa kuwa teknolojia inabadilika mara kwa mara.

Vile vile, taasisi zote za umma zinatakiwa kuweka taarifa za miradi ya TEHAMA inayoendelea katika mfumo wa Usimamizi wa Miradi ya TEHAMA Serikalini (Government ICT Project Portfolio) unaopatikana kwa anuani ya <https://gip.ega.go.tz>. Mfumo huu unaopokea na kutunza taarifa za miradi ya TEHAMA iliyopo na inayotarajiwa kuanzishwa Serikalini.

Pia, kwa wafanyabiashara wanaojihusha na miradi au utengenezaji wa mifumo ya TEHAMA Serikalini wanashauriwa kufuata orodha hakiki hiyo ili kujua mahitaji halisi ya Serikali na kuweza kujenga mifumo ya TEHAMA endelevu na inayoleta tija kwa umma

Wakala ya Serikali Mtandao (eGA), iliyoanzishwa 2012, ni taasisi ya Serikali yenye majukumu na mamlaka ya kuratibu, kusimamia na kukuza jitihada za Serikali Mtandao nchini Tanzania. Pia Wakala hii inasimamia udhibiti wa viwango vya Serikali Mtandao kwa kutumia Miongozo mbalimbali na Viwango vilivyowekwa ili kuwa na mifumo bora ya TEHAMA Serikalini.

XXXXXXXXXXXXXXXXXXXXXXXXXXXXMWISHOXXXXXXXXXXXXXXXXXXXXXXXXXXXX

Imetolewa Na:
Suzan Mshakangoto
Meneja Habari, Elimu na Mawasiliano
WAKALA YA SERIKALI MTANDAO (eGA)